**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI**


**NAMBA ZA SIMU**
**Mkuu wa Shule: 0787510607**
**Makamu Mkuu wa Shule :**
**0625800719/0784475860**
Email: josiahsosy@gmail.com



**Shule ya Sekondari Isaka,**
**S.L.P 119,**
**ISAKA - KAHAMA.**
**SHINYANGA.**
**Tarehe.........................**


**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
..............................................
..............................................
S.L.P....................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ISAKA, HALMASHAURI MSALALA, MKOA WA SHINYANGA MWAKA 2026-2027**

Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano (Form V) kwa mwaka wa masomo 2026/2027 katika Shule ya Sekondari **Isaka** iliyopo wilaya ya Msalala, Mkoa wa Shinyanga katika tahasusi (combination) ya .....................................kwa muda wote mwanao atakapokuwa katika shule hii,atapaswa kushirikiana na wanafunzi wenzake,walimu na wafanyakazi wasio walimu katika kutoa mchango wake wa mawazo na vitendo ili kuleta na kudumisha sifa na maendeleo ya shule hii kwa manufaa yake binafsi, wazazi/walezi na taifa kwa ujumla.

**MAHALI SHULE ILIPO.**

Shule ya Sekondari Isaka ipo kata ya Isaka katika Halmashauri ya wilaya ya Msalala, Mkoa wa Shinyanga.Shule ina maabara kwa masomo ya sayansi, umeme, maji n.k. Shule ipo kilometa 1.5 kutoka Bandari ya nchi kavu Isaka,Barabara kuu ya Tinde – Kahama.Upo usafiri wa pikipiki kutoka Isaka hadi shuleni nauli ni sh.2,000/=.

Kwa wanafunzi wanaotokea maeneo ya Kagera,Geita na Kigoma kupitia Kahama washukie Isaka, umbali kutoka hapo hadi mahali shule ilipo ni kilomita 1.5 ,Nauli kutoka **Isaka** hadi **shuleni** ni Tsh. 2,000/=

Kwa wanafunzi watokao Mwanza, Mara, Simiyu, Singida, Dar-es-Salaam,Morogoro,Dodoma, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara wapande Magari yanayoenda Kahama, washukie Isaka.

**Karibuni sana Isaka Sekondari.**

**...................................**

**KYARUZI E. RUGARABAMU**

**MKUU WA SHULE**

**PAMOJA NA BARUA HII NAAMBATANISHA TAARIFA ZIFUATAZO:-**

1. Fomu na 1 na 2 ambazo mnatakiwa mzijaze na mwanafunzi aje nazo shuleni.
2. Fomu na 3 ambayo ataipeleka kwa Daktari wa serikali ili apimwe afya yake na ailete shuleni.
3. Nakala ya sheria na kanuni za shule amabazo atatakiwa kuzisoma, kuzielewa na kuzizingatia.
4. Lugha ya mawasiliano na taaluma shuleni ni **KIINGEREZA** tu.

**TAREHE YA KUFUNGUA SHULE.**

Shule itafunguliwa kwa muhula wa kwanza mwezi wa saba tarehe .................. nafasi yako utakuwa umeipoteza mwenyewe kama hutaripoti mapema bila taarifa baada ya siku 30 tangu shule kufunguliwa.

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia.**

**2.1 Sare za Shule (School Uniforms).**.

**2.1.1 Wavulana**

a) Shati tatu (3) nyeupe za tetron zenye mikono mirefu na collar na ziwe ndefu kwa ajili ya kuchomekea.
b) Suruali aina tatu: Rangi Nyeusi kwa kushindia , light grey (1) na Dark green plain (1) .
c) Viatu vyeusi jozi mbili vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi (aje navyo).
d) Soksi jozi mbili (2) nyeusi ziwe ndefu (aje nazo).
e) Sweta la (maruni) mikono mirefu (aje nalo).
f) Nguo za michezo: fulana nyeusi, bukta nyeusi, viatu vya michezo au raba na soksi rangi ya bluu (aje nazo).

g) Nembo mbili (2) kwa ajili ya mashati ya shule, Tisheti mbili rangi ya dark bluu (2) Tshs 10,000/= kwa kila Tisheti. Tai mbili (2) Rangi ya Dark green. Vifaa hivyo vinapatikana shuleni.

h) Aje na kadi ya bima ya NHIF/ CHF, kwa ambaye hana kadi aje na shiringi elfu hamsini na mia nne tu (Tsh 50,400/=) kwa ajili ya bima ya Afya.

i) Tisheti mbili (2) za kushindia Rangi ya Kijivu za kora nyeusi zipo shuleni Tshs 10,000/= kwa kila Tisheti kwa atakayehitaji

**NB. RANGI YA VITAMBAA VYA SURUALI ZA SHULE NI;**



**NB: kama kiatu hakitakuwa cha kufunga kamba hakitakubaliwa.**

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo Mwanafunzi anapaswa kuja nayo Shuleni;

i. Madaftari kumi na nne (14) (QUIRE FOUR);
ii. Ream(A4) mbili (2) za karatasi kwa mwaka.(Double A au GSM)
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha iambatanishwe);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology
v. Godoro liwe na vipimo **$2\frac{1}{2}$ X 6.**
vi. Scientific Calculator;
vii. Mashuka Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (Rangi ya light blue).
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko
x. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xi. Kwanja1, jembe1, reki1, mifagio 2 wa ndani na wa nje.

## 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
| --- | --- | --- |

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: malipo yafanyike kupitia Bank ya NMB akaunti Namba 30601200131** (jina la akaunti ni **Shule ya Sekondari Isaka**).

**3. Sheria, kanuni na taratibu za shule.**

Shule ya sekondari Isaka inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu nchini. Hivyo mara ufikapo hapa shuleni utatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa walimu, viongozi , wazazi, wafanyakazi wasio walimu na wanafunzi wenzako.
ii. Kuhudhuria vipindi vyote darasani na katika shughuli mbalimbali za ndani na nje ya shule.
iii. Kuhudhuria masomo ya usiku (Preparation).
iv. Kuwahi katika shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia maelekezo kikamilifu ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, Mavazi na Mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
**xi.** Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au Kuishi kwenye Bweni ambalo hakupagiwa. Kitanda kimoja kitatumika kwa mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa)**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na;**

i. Wizi wa aina yoyote.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa ;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ Walezi na Jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga Mwalimu au mtu yeyote Yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usio kubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi, unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsia moja , kuoa/kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba ;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu,Siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

## 4. Viambatanisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazawa na Mganga Mkuu wa Hospital ya Serikali
ii. Fomu ya maelekezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na Sheria, Kanuni na Maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa Mwanafunzi wanaoweza kumtembelea Mwanafunzi Shuleni na Namba zao za Simu.

1. **TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule .…………………………………….**

**Muhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0787510607…………………………………….**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0625800719/0784475860…………………………………………...**
- **Mwandamizi Taaluma 0656335170/0769859975………………………………………………**
- **Mwandamizi Malezi …0684102065…………………………………....**

# KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI ISAKA

**MKUU WA SHULE. SHULE YA SEKONDARI ISAKA.**

**FOMU NA.1- HATI YA KUKUBALI KUSOMA NA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

**NYONGEZA A: AHADI YA MWANAFUNZI.**

Mimi.........................................................kutoka Shule ya Sekondari .......................................... nimekubali nafasi hii niliyopewa ya kujiunga na kidato cha .................................. katika shule hii. Naahidi nitatimiza wajibu wangu kwa uwezo wangu wote na kwa manufaa ya Taifa letu kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za shule. Na kwamba nitakuwa mtiifu na sitashiriki katika vitendo viovu kwa muda wote nitakao kuwa hapa shuleni. Nikikiuka sheria, kanuni na taratibu za shule, niadhibiwe inavyostaili na hata kufukuzwa shule.

**SAHIHI YA MWANAFUNZI................................ TAREHE............................**

**NYOGEZA B: AHADI YA MZAZI/MLEZI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI KULIPA MICHANGO YA SHULE NA MAELEKEZO MENGINE YA SHULE.**

Mimi....................................................... ambaye ni *mzazi/mlezi wa mwanafunzi ................................................................. wa kidato cha ........................ katika shule ya sekondari Mwalimu Nyerere, ninakiri kukubariana na sheria, kanuni kulipa gharama zote za shule pamoja na mahitaji mengine binafsi ya Mwanafunzi kwa lengo la kumwezesha asome katika mazingira mazuri. Pia napenda kuthibitisha kwamba mtoto wangu hatachelewa shuleni kwa kukosa mahitaji mbalimbali nimemaliza kukamilisha vifaa vyote vilivyoelekezwa hapo juu.

**SAHIHI YA * MZAZI/MLEZI.........................................** **TAREHE..................**

**NB: * Futa isiyohusika**

**FORM NO.3**

THE HEADMASTER,
ISAKA SEC. SCHOOL,
P.O.BOX 119,
KAHAMA.

**THE REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
TO THE MEDICAL OFFICER ......................................................................
**NAME OF STUDENT (IN FULL)..............................................................**

Please, kindly I ask you to examine the student named above as to his/her physical and mental fitness for fulltime study (two years course). The examination should include the following:

a) Eye – sight
b) Hearing
c) Speech
d) Limbs
e) Chest
f) Venereal diseases
g) Epilepsy
h) Leprosy
i) Cirrhosis
j) Other serious diseases
k) Pregnancy

**MEDICAL CERTIFICATE PART A:**
(To be completed by Government Medical Officer) I have fully examined the above named person and consider that he/she physically ***FIT/UNFIT** and mentally ***FIT/UNFIT** for a fulltime four two years study/course. (a) Eye- sight.........................................
(b) Hearing..................................................... (c) Speech............................................
(d) Limbs.............................................................. (e) Chest...............................................
(f). Venereal diseases............................................... (g). Epilepsy..................................
(h) Leprosy.................................................. (i) Neurosis.............................................
(j). Cirrhosis...........................................................................
(k). Other serious diseases......................................................................
(L). Pregnancy.....................................................................

# <u>OR0DHA YA VITABU VINAVYOHITAJIKA KULINGANA NA COMBINATION</u>

1. Madaftari 14 (counter book), Kalamu za wino, rula na Mathematics set.

2. Ream (Double A4) ya karatasi mbili (2) kwa mwaka, (ni lazima ikabidhiwe kwa msajili).

### A. HISTORY (walau vitabu viwili)

1. TIE (2023) History for Secondary Schools: Form Five - Tanzania Institute of Education.
2. . TIE (2023) History for Secondary Schools Form Six, Dar es Salaam: Tanzania Institute of Education
3. Tumaini, S.C.K (2020) Contemporary Historical Events: Advanced Level History one, Dar es Salaam: Shgibitali & Sons publishers

### B. ENGLISH LANGUAGE(walau vitabu viwili)

a) Animal farm (2024) George orwell East African Education publishers ltd.
b) Chasing the leopard finding the lion (2024) Julie Wakeman-Linn Mkuki na nyota publishers Ltd
c) The opportunist Elite (2023) Nyambari C. M. Nyangwine Mbesa Books Distributors
d) The Horizon Unveiled (2011) Fellowes Mwaisela FGD Tanzania Ltd
e) The Government Inspector (2024) Nkolai V. Gogol East African Educatioal Publishers Ltd
f) An Enemy of the people (2024) Henrik Ibsen East African Educational Pulishers Ltd
g) A Taste of Heaven (2023) Farouk Topan Mkuki na Nyota Publishers Ltd
h) SUMMONS: poems from Tanzania (2023) Richard. S. Mabala et al. Mkuki na Nyota Publishers
i) Poets of Africa; Lament of the silent & Other poems (2024) Jared Angira East African Educational Ltd

### C. LITERATURE IN ENGLISH (walau vitabu viwili)

a) Arrow of god (2024) Chinua Achebe East African Educational Publishers Ltd
b) A man of the people (2024) Chinua Achebe East African Educational Publishers Ltd
c) A Grain of Wheat (2023) Ngugi wa Thiong'o East African Educational Publishers Ltd
d) Petals of Blood (2023) Ngugi wa Thiong'o East African Educational Publishers Ltd
e) No Longer at Ease (2024) Chinua Achebe East African Educational Publishers Ltd
f) Joy Come in the morning (2023) Hopolang Phororo Mkuki na Nyota publishers Ltd
g) The lion of yola (2010) Sererone Ndunguru E &D Vision publishing
h) Betrayal in the City (2023) Francis Imbuga East African Educational Publishers Ltd
i) I will marry when I want (2023) Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Mirii East African Educational Publishers Ltd
j) Julius Caesar (2024) William Shakespeare East African Educational Publishers Ltd
k) Man of kafira (2024) Francis Imbuga East African Educational Publishers Ltd

### D. KISWAHILI (walau vitabu viwili)

a) Dunia Uwanja wa fujo (2023) Euphrase Kezilahabi Afica proper Education Network
b) Ua la faraja (2007) W. E. Mkufya Mangrove publishers
c) Mirathi ya Hatari (2023) C. G. Mung'ong'o Mkuki na Nyota pubishers Ltd
d) Wasifu wa siti Binti Saad (2023) Shaaban Robert Mkuki na Nyota pubishers Ltd

e) Mukwava wa Uhehe (2023) M. M. Mulokozi Afica proper Education Network
f) Shujaa mirambo (2023) Emmanuel mbogo Afica proper Education Network
g) Usaliti mjini (2024) Francis Imbuga (2024)
h) Fumbo linaendelea (2023) Nyambari C. M. Nyangwine Mbesa Books Distributors
i) Malenga wa Ziwa kuu (2024) Wallah Bin Wallah (2024) East African Educational Publishers Ltd
j) Andamo,Msafiri safarini (2023) Mohammed Khelef Ghassani Educational Books Publishers Ltd
k) Wosia wa Baba (2024) Ahmed Mohamed Amanzy Abantu publuications Ltd
l) Vuta n'kuvute (2007) Shafi Adam Shafi Mkuki na Nyota pubishers Ltd
m) Asali chungu (2024) Said Ahmed Mohamed East African Educational Publishers Ltd
n) Mwana wa yungi Hulewa (20230 Mohammed Said Abdulla East African Educational Publishers Ltd
o) Vupuli vya Figo (2024) Emmanuel Mbogo East African Educational Publishers Ltd
p) Kaptula la Marx (2023) Euphrase Kezilahabi Africa Proper Education Network
q) Nyerere na Safari ya kanaani (2023) Emmanuel mbogo Africa Proper Education Network
r) Moran (2007) Emmanuel mbogo Africa Proper Education Network
s) Dhifa (2023) Euphrase Kezilahabi Africa Proper Education Network
t) Utenzi majumui wa karne ya 21 (2023) Idd m, Mwimbe Nyambari Nyangwine publishers
u) Malenga wa Bara (2023) M. M Mulokozi na KI. K Kahigi Africa Proper Education Network
v) Fungate ya Uhuru (2007) Mohamed Self Khatibu Africa Proper Education Network

**E. GEOGRAPHY (walau vitabu viwili)**

a) Geography for secondary school form five and six TIE (2023)
b) Practical geography – khallar DR (2022)
c) Physical geography in diagram –bunnet
d) Geomorphology (3rd ed) – singhs (2022)
e) Map reading and phography interpretation 2018-Rashid S.M